

Je, kwa nini watu waanzao kutumia dawa za kulevya hupenda kuendelea kuzitumia?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Hii ndio hasa sababu kwa nini dawa za kulevya ni hatari! Mara unapozioea unakuwa na ugumu wa kuendesha maisha yako bila dawa za kulevya. Kwa dawa nyingi za kulevya ubongo huzoea kuwepo kwake kwenye damu na dawa zaidi na zaidi huhitajika i ili kuendeleza hali hiyo. Hii i ii ina maana kadri muda unavyoenda ndivyo unavyoongeza kiasi cha dawa za kulevya unachokihitaji. Pale utakapotaribu kupunguza kiasi cha matumizi ya dawa za kulevya au kuacha kabisa unaweza kupata hali ya kimaumbile au kiakili i i itokeayo kutokana na kuacha kitu ulichozoea. Hali hii inaweza i isiwe ya kufurahisha, yenye kuumiza na pengine hatari kwa maisha yako. Mara mtu anapozioea dawa za kulevya haiwi tu tabia bali ugonjwa. Watu wengi wanaotegemea dawa za kulevya hawazitumii kwa kujifurahisha bali kuzuia maumivu yasababishwayo na kuacha kitu ulichozoea. Njia nzuri ya kuzuia hali hii ni rahisi: kuwa jasiri na sema HAPANA. Usijaribu dawa za kulevya.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25845>